**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI**

**MANISPAA YA GEITA**

SHULE YA SEKONDARI NYANKUMBU,
S.L.P140,
**GEITA**
……………

.

**NAMBA ZA SIMU**
MKUU WA SHULE 0756 735 250
MAKAMU MKUU WA SHULE 0684 945 989/ 0767 677 242

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………..………………………

**1.0 UTANGULIZI**

1.1 Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana NYANKUMBU katika Kidato cha Tano **………...**
Kwa niaba ya Bodi ya shule,Walimu, Wafanyakazi na wanafunzi wa shule hii, nakupongeza na kukukaribisha kwa moyo wa dhati na kindugu.
Shule hii ipo Umbali wa **Kilomita 6** Kusini mwa **Halmashauri ya Manispaa GEITA.** Usafiri wa Bajaji/Pikipiki kutoka kituo cha Mabasi Geita Mjini (Stendi Kuu) Unapatikana.

1.2. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **………….** Unatakiwa kuripoti shuleni kwa wakati ndani ya siku saba.

1.3 Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii zote, kufuata Kanuni,Taratibu na Sheria za Shule na kushiriki katika Mipango ya Elimu ya kujitegemea. Shughuli zozote utakazozifanya shuleni hapa zinatahiniwa kila siku na ni sehemu ya Mtihani wa Kidato cha Sita.

1.4 Kuchaguliwa kwako kujiunga na kidato cha tano ni **BAHATI**. Hivyo una **DENI** Kubwa kwa Nchi yako, Serikali yako na ni kama umetumwa na wananchi walio Vijijini/ Kijijini kwako ulikotoka. Hivyo wanakutegemea uvune chochote Shuleni na hatimaye urudi kuwasaidia ukishavuna ulichopanda.

1.5 (a) Shule hii ni MAALUMU kwa wanafunzi wa KIKE tu, wanafunzi wanasoma kwa bidii kwa malengo ya kupata ufaulu wa **DIVISHENI 1** . Ni jukumu lako Mzazi kuhakikisha kuwa mwanao anapata mahitaji yake ya lazima ili apate muda mrefu wa kujisomea kwani Elimu ya **Advanced-Level** inahitaji mwanafunzi ajitafutie maarifa zaidi, akiongezea kwa kile anachopatiwa na mwalimu.

(b) Ikumbukwe kuwa jukumu la kuwalea wanafunzi ni letu sote; Wazazi na walimu, kwa hiyo unapohitajika hapa shuleni lazima ufike kuangalia tabia, maendeleo ya mwanao kitaaluma na mwenendo wake. Kushindwa kuitikia wito wa shule kunaweza kusababisha mwanao kusimamishwa masomo na hata wewe kuchukuliwa hatua za kisheria.

(c) Uhamisho usio wa lazima au holela kwa wanafunzi wa shule hii hautakubaliwa. Uhamisho utakaotolewa ni ule wa lazima na halali wenye viambatanisho vya sababu za kuomba uhamisho huo; nao utatolewa mara mbili kwa mwaka yaani mwezi Juni na Desemba.

Hivyo utaijulisha shule mapema ili taratibu za uhamisho zifanyike kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia.

(d) Ni kosa **kisheria** kwa mzazi /mlezi kumuozesha mwanae akiwa bado ni mwanafunzi. Mwanao lazima amalize shule. Ni haki yake ya msingi na ya kikatiba wewe mzazi kumsomesha na Kumgharamia mahitaji yote ya shule pamoja na MATIBABU.

(e) Ili tuweze kupashana habari juu ya maendeleo ya mwanao, itakubidi kujulisha shule Anuani/ Namba ya SIMU yako Kamili, hii ni pamoja na unapobadilisha Anuani/Namba ya SIMU.

(f) Mwanao akishajiunga na shule hii atalazimika kushiriki shughuli zote za shule bila kujali matakwa ya Mzazi/Mlezi wake.

(g) Wakati mwanao akiwa mwanafunzi wa shule hii atashiriki na kuhudhuria michezo shuleni na hivyo awe na nguo za michezo kwa ajili ya mazoezi.

(h) Mwanao atalazimika kuhudhuria siku zote **194** za masomo, kama itatokea shida yoyote ya lazima kutofika shuleni, utatoa taarifa ya maandishi.. Pengine unaweza kufika mwenyewe kumuombea ruhusa.

(i) Sababu kubwa ya mwanao kuwepo shuleni ni kusoma kwa bidii na kufaulu Mitihani yote ya **Ndani** na **Nje** ya shule kwa **Kiwango cha Wastani wa A au B**. Mzazi/Mlezi hakikisha mwanao anahudhuria masomo yote na kuyafaulu kwa Gredi A au B.

(j) Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza au Kiswahili inapobidi.

(k) Katika jamii yoyote ile wakosaji huchukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu. Hapa shuleni adhabu hutolewa kwa wakosaji wa nidhamu vilevile. Hivyo Mzazi/Mlezi hataruhusiwa kuingilia hatua za kinidhamu zinazochukuliwa dhidi ya wakosaji. Kufanya hivyo kunaweza kusababisha mwanao kupoteza nafasi hii aliyopewa. Hali kadhalika kama mwanao atakataa adhabu yoyote aliyopewa anaweza kupoteza nafasi yake kwa mujibu wa sheria za shule.

(l) Ni jukumu lako Mzazi kuhakikisha kuwa mwanao anaishi maisha ya uanafunzi anapokua nje ya shule yaani nyumbani. Shule haitasita kumchukulia hatua za kinidhamu dhidi ya utovu wa nidhamu nje ya shule. Anatakiwa kubaki ni mwanafunzi wakati wowote awe shuleni au nje ya shule.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA 1.1 SARE YA SHULE

a) Mashati mawili (02) meupe ya Tetroni yenye mikono mirefu
b) Sketi mbili (02) bluu bahari (GRADE ONE/ Na.1) zenye malinda 6 - yanapangwa matatu matatu kila upande yakitazamana, kulia na kushoto, mbele na nyuma hakuna malinda, Mkanda wake inchi 2 na Urefu inchi 8 kutoka kwenye magoti /Sketi ndefu. Pia unaweza kushonea shuleni; fundi yupo.

c) Tai moja inapatikana shuleni
d) Sweta moja bluu inapatikana shuleni
e) Viatu vyeusi vya ngozi ( Kisigino butu )
f) Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (02) au zaidi
g) T- shirt yenye nembo ya shule “dark blue” yenye kola ya kaki na Ufito wa kaki inapatikana shuleni
h) ‘Track suit’ rangi ya kijivu kwa ajili kusomea usiku (Prepal)
i) ‘Track suit’ rangi ya kijani kwa ajili ya michezo
j) Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo.
k) Shamba “dress” –Gauni la kushindia la HESHIMA (Kitambaa cha Kunguru/’tetron’ ya Draft ndogo rangi ya Kijani).
l) Mwanafunzi anaruhusiwa kusuka nywele 5 mpaka 7 maarufu kama UTII WA RODA au TWENDE KILIONI.

**Aidha**, Kwa wale watakaoshindwa kupata mahitaji ya sketi,Tai na shamba dress kwa kitambaa sahihi, mahitaji hayo pia yatapatikana Shuleni.

**NB**: Mwanafunzi **haruhusiwi** kuja na Suruali, Pedo na nguo nyingine zinazofanana na hizo. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni

## 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAYO SHULE A. VIFAA VYA MASOMO

i. Daftari kubwa 10 (2 quire au 3 quire) pia zinapatikana kwenye Duka la shule
ii. Kalamu za kutosha.
iii. Mkebe mmoja wa vifaa vya ADVANCED MATHEMATICS na BAM
iv. Dictionary (OXFORD ADVANCED LEARNERS DICTIONARY) kwa **HKL**.
v. Aje na **Ream** mbili (A4) aina ya **Double A** , hizi ni karatasi kwa ajili ya mitihani
. mbalimbali .
vi. Faili moja (Folder File)
vii. Scientific Calculator – kwa PCM, CBG na PCB.
viii. Dissecting Kit kwa Wanafunzi wa CBG na PCB

### B. VIFAA VYA USAFI:

i. Ndoo moja ya lita 10 kwa ajili ya matumizi yake binafsi.
iii. Squeezer ( kikaushio maji)
iv. JEMBE 01, FYEKEO 01, HARD BROOM 01, SABUNI YA MAJI LITA 01, kwa wanafunzi wa Tahasusi ya PCB na CBG
v. FYEKEO 01, JEMBE 01, BRASH ZA KUSUGULIA CHOONI (VIFAGIO VIFUPI VYA KUSAFISHIA CHOONI 01), SABUNI YA MAJI LITA 01 kwa wanafunzi wa Tahasusi ya PCM na HKL

### C. VIFAA VYA BWENI

i. Godoro jipya futi mbili na nusu $2^1/_2 \times 6$, aina ya” **Comfy” au “Super Banco**”
ii. Shuka 02 rangi ya bluu bahari
iii. Foronya 02 za bluu bahari na mto wake
iv. Blanketi 01
v. Neti moja futi 4, rangi nyeupe pembe nne (4)
vi. Sanduku la chuma na kufuli lake.

vii. Nguo ya kulalia ( night dress)
viii. Taulo, Kitenge/ Khanga ( pair moja ), Kandambili, sabuni za kutosha, miswaki, dawa ya meno kubwa, soap dish, vibanio vya kuanika nguo
ix. Tochi au taa ya sola kwa dharura
x. Vyombo vya chakula sahani, kijiko, kikombe, na chombo cha kutunzia maji ya kunywa
xi. Viatu vya wazi jozi 02 (open shoes).
xii. SABUNI YA MAJI LITA 1

**2.3 MICHANGO YA SHULE**

| | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| 5 | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** *Michango yote ilipwe kwenye Nyankumbu S.S A/C NA.* ***31003300026*** *Benki NMB. Tafadhali, hakikisha unaandika Jina kamili la Mwanafunzi husika wakati wa kufanya malipo Benki.* ***MICHANGO HII HAPO JUU ILIPWE BENKI***

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanunl za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shu Ie;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shu Ie;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuteni kwa namna yoyote lle,na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuteni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.(Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahuslano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa:
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa; xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

**A. FOMU YENYE MAELEZO JUU YA AFYA:**

- Pamoja na barua hii fomu yenye maelezo kuhusu afya ya mwanafunzi imeambatanishwa ikikutaka ukapime afya yako katika hospitali ya Serikali.

**B. FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI:**

- Imeambatanishwa Mzazi/ Mlezi na mwanafunzi waijaze kwa ukamilifu na kuileta shuleni siku tajwa ya kuripoti

**C. BIMA YA AFYA/NHIF**

- Mwanafunzi aje na KADI ya Bima ya Afya ya NHIF au SH.50,400/= kwa ajili ya kukatiwa BIMA YA AFYA; Shuleni

**D. SHERIA ZA SHULE:**


- Sheria za shule zimeambatanishwa.

**F. Picha nne (4)** za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao

**NB: Simu za mkononi haziruhusiwi shuleni. *Ukikamatwa na simu utafutwa shule*.**

Nakutakia maandalizi mema

**KARIBU SANA NYANKUMBU SEKONDARI**



**GEITA TOWN COUNCIL**

**NYANKUMBU GIRLS SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a Medical Officer in respect of Nyankumbu Girls Secondary school

1. Full Name of Student………………………………………………………………..
2. Sex…………………………………………………………………………………..
3. HGB TEST………………………………………………………………………….
4. STOOL……………………………………………………………………………..
5. URINE TEST……………………………………………………………………….
6. T.B TEST……………………………………………………………………………
7. EYE EXAMINATION……………………………………………………………….
8. E.N.T………………………………………………………………………………..
9. CHEST……………………………………………………………………………….
10. ABDOMEN…………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**

Physical defects or impairments, infections, chronic or heredity (family disease).

………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above student and considered that; she is physically / not physically fit for studies.

Name…………………………………………………. Signature………………………

Date………………………….

**OFFICIAL STAMP**

**HALMASHAURI YA MANISPAA GEITA**
**SHULE YA SEKONDARI NYANKUMBU**
**FORM YA KUANDIKISHWA SHULE**
**(Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa Mkuu wa shule )**

1.0 Jina la Mwanafunzi ……………………………………Tarehe ya kuzaliwa……………………

Wilaya……………………………Mkoa……………………..Taifa……………………….................. Shule ya Sekondari unayotoka………………………………………………………………………… 1.1 Jina la Mzazi / Mlezi (wa kiume)……………………………………………………… Namba ya simu……………………………………………………………………….. Anwani yake……………………………………………………………………….

**PICHA MZAZI WA KIUME**

Kazi ya Mzazi / Mlezi…………………………………………………………………………………

1.2 Jina la Mzazi / Mlezi (wa kike)………………………………………………………… Namba ya simu…………………………………………………………………………….. Anwani yake……………………………………………………………………………….. Kazi ya Mzazi / Mlezi…………………………………………………………………..

**PICHA MZAZI WA KIKE**

2.0 Jina na anwani ya jamaa yako anayeishi karibu na shule hii (kama yupo)

**PICHA NDUGU WA KIUME**

2.0……………………………………………………………………………………………

**PICHA NDUGU WA KIKE**

2.1……………………………………………………………………………………………

3.0 **AHADI ZA MWANAFUNZI.**

(a) Mimi ……………………………………………..Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote ambayo ni pamoja na sheria za shule na nimekubali kuingia kidato cha Tano katika shule ya Sekondari ya wasichana Nyankumbu kuanzia…………………………….

(b) Kwa hiyo naahidi kwamba.

i. Nitatimiza sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa ii. Stashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina la Mwanafunzi………………………….. ……Sahihi……………………Tarehe……..….

4.0 **AHADI YA MZAZI /MLEZI**

Mimi ……………………………Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi……………………….............

4.1 Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu kwa ujumla katika kumwelimisha na kumlea motto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa atazitii sheria zote za shule na kuyatimiza mambo yote yote yaliyotajwa.

4.2 Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni siku ya shule bila kuchelewa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya maandishi pale mwanafunzi atakapokuwa na tatizo la kumfanya asihudhulie masomo.


Jina la Mzazi / Mlezi………………………….. ……Sahihi……………………Tarehe……..….

**5.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE** (i) Wizi

(ii) Kitohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wasiosuka wanatakiwa kuwa na nywele fupi zisizozidi sm 5 wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo ulioelekezwa na Uongozi wa shule.
(vii) Uvutaji wa sigara na madawa ya kulevya kwa ujumla wake.
(viii) Uasherati,mapenzi ya jinsia moja au kuolewa
(ix) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(x) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi;
(xi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xii) Kumiliki na kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiii) Kudharau bendera ya Taifa
(xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua.
(xv) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**6.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule **0756 735 250**
- Makamu Mkuu wa Shule **0767 677 242 /0684 945 989**
- Mwandamizi Taaluma **0765 562 205**
- Mwandamizi Malezi **0786 771 775 / 0767 939 206**